

# Habari za COVID-19 kwa New Mainers

- 1.** Kuanzia kesi 1 mnamo tarehe 12 Machi sasa tuna kesi zaidi ya 100 huko Maine hivi leo.
- 2.** COVID-19 (Virusi vya Korona) ni ugonjwa mbaya na unaenea sana huko Maine. Ugonjwa huu ni halisi!
- 3.** Tunaomba tafadhali uheshimu na ufuate mwongozo wote ili kusaidia kumaliza kuenea kwa virusi katika jamii yako.
- 4.** Tafadhali jiweke wewe, familia yako na jamii yako salama wakati wote. Usimruhusu mtu yeyote nyumbani kwako isipokuwa watu ambao wanaishi humo.
- 5.** Nawa mikono yako mara kwa mara na uepuke kugusa watu au kitu chochote kadiri iwezekanavyo. Nawa mikono yako mara tu baada ya kugusa kitu chochote.
- 6.** Kaa nyumbani kadiri iwezekanavyo. Epuka kuchukua wanafamilia na marafiki wako kwa ununuzi wa mboga. Watoto wanapaswa kutoenda kwa uwanja wa michezo.
- 7.** Epuka kukusanyika katika vikundi vya watu zaidi ya 10 iwe nyumbani au hadharani. Kujitenga na wenzio hakumaanishi kutembelea nyumba za marafiki/familia na kukaa chini ya futi 6 kutoka kwa kila mmoja.